

VYANZO VYA MAGONJWA AMBUKIZI

"Gavana wa jimbo hili, waziri wa afya, maafisa wa siha katika gatuza letu, mabibi na mabwana, hamjambo? Mwaambaje? Nina matumaini si haba kuwa nyote m wazima. Isitoshe, nimejawa na furaha tele kuwaona mkiwa mmejumuika katika uwanja huu ili kufahamu mliloitiwa. Huo ndio moyo wa uzalendo. Endeleeni na moyo uo huo.

Sababu ya kukusanyika katika uga huu ni kufahamishana kuhusu vyanzo vya magonjwa ambukizi. Je, magonjwa ambukizi ni magonjwa gani? Yamkini unajiuliza swali hilo. Haya ni maradhi yanayoweza kusambaa kutoka kwa mtu mmoja hadi kwa mwingine. Bila shaka, wengi mngenda kujua kinachosababisha magonjwa haya na jinsi yanavyosambaa. Kulifahamu hili kutatuwezesha kuyazuia.

Magonjwa ambukizi huweza kusababishwa na uchafu. Ulaji wa chakula kichafu, unywaji wa maji machafu na kufanyia kazi katika mazingira machafu huweza kusababisha maradhi kama vile kichocho, kipindupindu, kuendesha na mengineyo. Ndwele hizi huletwa na viini vinavyopatikana katika uchafu. Aidha, viini hivyo husambazwa na vimelea au wadudu wapendao uchafu kama vile nzi, mende na chawa.

Chanzo kingine cha magonjwa haya ni kupumua hewa iliyochafuka. Baadhi ya magonjwa husambazwa kupitia hewa yenye viini vinavyosababisha ugonjwa. Magonjwa haya ni kama vile korona, kukohoa, kifua kikuu na kifaduro. Maradhi hayo husambaa ukipumua hewa yenye viini hivyo. Hii ina maana kuwa, ni vyema kuwa katika mazingira yanayoruhusu mzunguko mzuri wa hewa. Watu wanapokohoa au kupiga chafya, wahakikishe kuwa wanafanya hivyo katika mazingira yaliyo wazi.

Isitoshe, magonjwa ambukizi huweza kutokana na kutopewa chanjo. Kuna magonjwa ambukizi kama vile ukambi, kifua kikuu na kupooza ambayo huweza kuzuiwa kwa kupewa chanjo. Yeyote asiyepewa chanjo kwa wakati na njia inayofaa huweza kuathiriwa na magonjwa hayo.

Kupewa chanjo huusaidia mwili wa mtu kujenga kinga ya kukabiliana na magonjwa hayo yanapotokea.

Pia, maradhi mengine huambukizwa kupitia wadudu. Ugonjwa kama vile malaria husambazwa na mbu. Malale nao huweza kusambazwa na mbung'o. Viroboto na panya husambaza tauni bila kusahau chawa ambao husambaza kipwepwe. Visalisali ni vidudu vinavyopatikana katika konokono. Visalisali husambaza kichocho.

Ninaomba kukomea hapo ili nisiwachoshe na mengi. Ni vyema kufahamu kuwa jukumu la kudhibiti magonjwa ambukizi ni letu sote. Magonjwa ni mzigo mkubwa na chanzo cha gharama kwa mtu binafsi, familia na nchi kwa jumla. Afya ni tunu. Afya ni dhahabu. Afya ni bora kuliko mali."